

TANGAZO KWA UMMA

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania inautangazia umma kuwa imepanga kuwakopesha wavuvi mkopo nafuu (usio na riba) wa Boti za "*Fiber*" za Uvuvi awamu ya tatu. Mkopo huu unalenga kuwawezesha wavuvi kufanya uvuvi wa kibiashara.

Boti za urefu wa kuanzia mita 5 - 14 na injini zake zenye nguvu ya farasi (HP) kama ifuatavyo; mita 5 injini ya 9.9HP, mita 8 na 10 injini ya 15HP, mita 12 na 14 injini ya 60HP; uwezo wa kubeba wavuvi 6 hadi 20; uwezo wa kubeba samaki tani 2.0; kifaa cha kuongozea boti (GPS); vifaa vya kuokolea maisha; kifaa cha kuzimia moto; boti 2 saidizi kwa boti za mita 12 na 14; nyavu na vifaa vyake.

Miongozo ya maombi na vigezo vya kina vinapatikana kwa Wakurugenzi wa Halmashauri husika kupitia Afisa Uvuvi wake, Ofisi za Kanda za Sekta ya Uvuvi au tembelea www.mifugouvuvu.go.tz

Wananchi walio tayari kukopa wawasilishe maombi yao Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika. Maombi hayo yawasilishwe kabla ya tarehe 16 Januari 2026 kupitia anuani ifuatayo:-

KATIBU MKUU
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
S.L.P 2847
40487-DODOMA
Simu: +255 26 23 22613
Barua pepe: ps@mlf.go.tz

Maelezo ya Ziada ya Tangazo la boti awamu ya III

Maombi yazingatie urefu wa boti, aina ya Uvuvi unatarajiwa kufanyika, na maeneo ya uvuvi kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Na.	Urefu wa boti	Ukanda wa Uvuvi	Aina ya uvuvi
1	Mita 14, Injini ya 60HP	- Pwani, - Ziwa Tanganyika, - Ziwa Nyasa	Ringnet (Dagaa na Samaki)
	Mita 12, Injini ya 60HP	- Pwani, - Ziwa Tanganyika, - Ziwa Nyasa	Ringnet (Dagaa na Samaki)
	Mita 10, Injini ya 15HP	Ziwa Victoria,	Uvuvi wa Dagaa
	Mita 8, Injini ya 15HP	Ziwa Victoria, Maji madogo (Mtera, Nyumba ya Mungu, Babati, Manyara, Singidani, na Ikimba)	Uvuvi wa Sangara na Samaki wengine
	Mita 5, Injini ya 9.9HP	Pwani, Victoria, Tanganyika, Nyasa	Kuhudimia shughuli za ukuzaji wa viumbe maji ikijumuisha ufugaji wa Samaki kwa njia ya vizimba, jongoo bahari, na kilimo cha Mwani)

Vigezo:



WIZARA YA
MIFUGO NA
UVUVI

TADB
Benki ya Maendeleo
ya Kilimo Tanzania
"Benki ya Wakulima"

MAHITAJI YA MAOMBI YA MKOPO KWA KIKUNDI (CBO) AU CHAMA CHA USHIRIKA (FICO)

1. MAMLAKA YA KUKOPA

- (a) Barua ya maombi ikiainisha mahitaji ya mkopo, madhumuni ya mkopo, chanzo/vyanzo vya marejesho ya mkopo na muda wa marejesho.
- (b) Muhtsari wa kikao cha mkutano mkuu kilichoidhinisha kukopa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ukiambatana na Mahudhurio ya washiriki pamoja na sahihi zao.
- (c) Nakala ya kitabu cha usajili wa wanachama (rejesta ya wanachama wote).

2. UHALALI WA MKOPAJI

- (a) Cheti cha usajili wa chama cha ushirika au kikundi
- (b) Katiba ya chama iliyosajiliwa.
- (c) Cheti cha ukomo wa madeni na makisio yaliyopitishwa na ofisi ya ushirika (kwa vyama vya ushirika tu).
- (d) Barua ya udhamini wa kikundi toka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri (kwa vikundi tu).
- (e) Leseni ya kujishughulisha na uvuvi na mazao yake.
- (f) Kibali cha ukuzaji viumbe maji.

3. TAARIFA ZA KINA JUU YA MRADI

- (a) Mpango wa Biashara (Business Plan)
- (b) Wasifu wa viongozi wa chama.
- (c) Taarifa ya uzalishaji (kama ipo).
- (d) Mkataba wa kuuza mazao ya uvuvi kwa mnunuzi mwenye uwezo na ambaye chama kimeridhia (kama upo).

4. TAARIFA ZA FEDHA

- (a) Akaunti ya Benki.
- (b) Taarifa ya Benki kwa miezi kumi na mbili (12) ya hivi karibuni (kama ipo).
- (c) Makadirio ya mtiririko wa fedha/Makadirio ya mapato na matumizi.
- (d) Taarifa za ukaguzi wa fedha za chama kutoka COASCO (kwa vyama vya ushirika).
- (e) Taarifa ya mikopo yote ya nyuma na ya sasa ambayo chama kiliwai kukopa/inadaiwa na taasisi yoyote ya fedha au Halmashauri (mikataba ya mikopo iambatanishwe).

5. TAARIFA JUU YA DHAMANA ZA MKOPO

Dhamana kwa vyama vya ushirika na vikundi itakuwa kupitia Halmashauri au malli za chama cha ushirika na kikundi husika.





WIZARA YA
MIFUGO NA
UVUVI

TADB
Benki ya Maendeleo
ya Kilimo Tanzania
"Benki ya Wakulima"

MAHITAJI YA MAOMBI YA MKOPO KWA KAMPUNI

1. MAMLAKA YA KUKOPA

- (a) Barua ya maombi ikiainisha mahitaji ya mkopo, madhumuni ya mkopo, chanzo/vyanzo vya marejesho ya mkopo na muda wa marejesho.
- (b) Muhtsari wa kikao cha bodi kilichoidhinisha kukopa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

2. UHALALI WA MKOAJI

- (a) Hati ya Usajili (Certificate of Incorporation),
- (b) Memorandum and Articles of Association (MEMART),
- (c) Leseni halali ya Biashara (valid Business licence),
- (d) Namba ya mlipa Kodi (TIN Certificate),
- (e) Cheti cha mlipa kodi (Tax Clearance Certificate),
- (f) Cheti cha Usajili wa VAT (VAT Registration Certificate),
- (g) Taarifa sahihi ya kampuni kutoka kwa Msajili wa Makampuni (Recent Official Status from Registrar of Companies).
- (h) Leseni ya kujishughulisha na uvuvi na mazao yake.
- (i) Kibali cha ukuzaji viumbe maji.

3. TAARIFA ZA FEDHA

- (a) Andiko la Mradi (detailed Business plan).
- (b) Mrejesho/Ripoti ya mwenendo wa biashara wa mwaka uliosajiliwa kwa Msajili wa makampuni (Annual Returns filed with Register of Companies).
- (c) Ripoti ya ukaguzi wa fedha ya miaka mitatu (audited financial statements for at least past three years).
- (d) Makadirio ya matumizi/mtiririko wa fedha (cashflow projections).
- (e) Hifadhi ya bidhaa na madeni ya Kampuni (Stock and debtors position - age-wise).
- (f) Taarifa ya mikopo yote ya nyuma na ya sasa ambayo kampuni iliwai kukopa/inadaiwa na taasisi yeyote
- (g) ya fedha au Halmashauri (mikataba ya mikopo iambatanishwe).
Taarifa ya Benki ya miezi kumi na mbili (Bank statement for the past twelve months).
- (h) Historia na maelezo kuhusu kampuni (taarifa ya umiliki, wasifu wa viongozi na Bodi).
- (i) Nakala ya vitambulisho vya wakurugenzi na menejimenti ya kampuni (ambatanisha kitambulisho cha Taifa au kadi ya mpiga kura).
- (j) Mikataba ya wanunuzi na wasambazaji (ambatanisha nakala za mikataba kama ipo).

4. TAARIFA JUU YA DHAMANA ZA MKOPO

- a) Aina na nakala za hati na dhamana zitakazotolewa.
- b) Thamani ya dhamana zitakazotolewa (Valuation Report).





WIZARA YA
MIFUGO NA
UVUVI

TADB
Benki ya Maendeleo
ya Kilimo Tanzania
"Benki ya Wakulima"

MAHITAJI YA MAOMBI YA MKOPO KWA MTU BINAFSI

1. MAMLAKA YA KUKOPA

- (a) Barua ya maombi ikiainisha mahitaji ya mkopo, madhumuni ya mkopo, chanzo/vyanzo vya marejesho ya mkopo na muda wa marejesho.
- (b) Awe Mtanzania mwenye umri zaidi ya miaka kumi na nane (ambatanisha nakala ya kitambulisho cha Taifa au kadi ya mpiga kura).
- (c) Barua ya utambulisho wa makazi toka Serikali ya Mtaa au uongozi wa BMU.
- (d) Awe amedumu kwenye uvuvi kwa muda usiopungua miaka mitatu na kuendelea.

2. UHALALI WA MKOPAJI

- (a) Leseni halali ya Biashara (valid Business licence).
- (b) Namba ya mlipa Kodi (TIN Certificate).
- (c) Cheti cha mlipa kodi (Tax Clearance Certificate).
- (d) Cheti cha Usajili wa VAT (VAT Registration Certificate).
- (e) Leseni ya kujishughulisha na uvuvi na mazao yake.
- (f) Kibali cha ukuzaji viumbe maji.

3. TAARIFA ZA KINA JUU YA MRADI WA UVUVI NA FEDHA

- (a) Mpango wa Biashara (detailed Business Plan).
- (b) Taarifa ya benki kwa miezi kumi na mbili.
- (c) Taarifa za Uvuvi zinazohusu mapato na matumizi.
- (d) Taarifa ya kina ya jinsi mradi husika utakavyonufaisha jamii (ajira kwa vijana na manufuaa mengine kwa jamii).
- (e) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa uvuvi haramu au makosa mengine ya uvuvi.

4. TAARIFA JUU YA DHAMANA ZA MKOPO

- (a) Aina na nakala za hati na dhamana zitakazotolewa.
- (b) Thamani ya dhamana zitakazotolewa (Valuation Report).

